# HAKI ZA WATOTO




**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**
**DAR ES SALAAM.**

# HAKI ZA WATOTO

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA
DAR ES SALAAM.

**SHUKURANI**

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inawashukuru wote wale waliohusika kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha utoaji wa kitabu hiki. Shukurani nyingi zinatolewa kwa wafuatao waliohusika na uandishi wa kitabu hiki.

| | |
|---|---|
| Dk. K. Mtebe | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| Ndugu W.I. Mjema | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| ,, G. Lubega | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| ,, E. Delem | UMATI Makao Makuu |
| ,, J.C. Kasambala | UMATI Makao Makuu |
| ,, A. Mwambogela | Taasisi ya Ukuzaji Mitaala |
| ,, A. Semoka | UMATI Morogoro |
| ,, I. Tukai | Ustawi wa Jamii, Makao Makuu. |

Kiongozi wa warsha:

| | |
|---|---|
| Ndugu Laurence Kagaruki | Mkuu wa Idara<br>Elimu kwa Umma<br>Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima<br>Dar es Salaam |

## YALIYOMO

Sura ya Kwanza
HAKI YA KUTUNZWA KIMWILI ................1
Sura ya Pili
HAKI YA KUPENDWA NA KUKUBALIKA ..........................................10
Sura ya Tatu
HAKI YA USALAMA NA KUVUMILIWA ..........................................1..
Sura ya Nne
HAKI YA KUJIFUNZA .............................17
Sura ya Tano
HAKI YA KUTENDA NA KUJIELEZA ..........................................23
Sura ya Sita
HAKI YA KUONGOZWA NA KUKUBALIWA ..........................................27
Sura ya Saba
HAKI YA MTOTO KIKATIBA NA KISHERIA ..........................................30

## UTANGULIZI

Kitabu hiki kimeandikwa kwa ajili ya wazazi na wengine wote ambao wanahusika na malezi ya watoto. Pia kinafaa kusomwa na wote wanaojiandaa kupata mtoto au watoto.

Kitabu hiki kinaeleza kwa undani kuhusu haki za mtoto. Haki za mtoto ni kutunzwa kimwili, kupendwa na kukubalika, kuwa salama na kuvumiliwa, kujifunza, kutenda, kujieleza, kuongozwa na kushauriwa. Pia kinaelezea juu ya mtoto kulindwa kikatiba na kisheria.

Tunatumaini kuwa kitabu hiki kitakuwa msaada mkubwa katika kuwalea watoto wetu.

Wanawarsha

Mei 1988

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima 1988

Msanii: G.G. Kiiza

Haki zote za kunakili zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kunakili au kukitoa katika hali yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

# Sura ya Kwanza

## HAKI YA MTOTO KUTUNZWA KIMWILI

Mtoto ana haki ya kutunzwa kimwili na wazazi au walezi wake. Ni makosa kwa wazazi kumnyima mtoto haki hii. Hivyo ni wajibu wa wazazi kuhakikisha kuwa mtoto anapata lishe bora, afya na malazi bora.

**LISHE**

Mtoto apewe chakula kwa sababu ni haki yake. Chakula bora ni muhimu kwa maisha ya mtoto ili aweze kukua kimwili na kiakili.



*Kielelezo 1.1*

**Madhara yatokanayo na Kukosa Lishe Bora**

Magonjwa mengi humpata mtoto kwa sababu ya kutokula chakula cha kutosheleza mwili. Mtoto asipopata shibe

ya kutosha anaweza kupata matatizo yafuatayo:-


- Kushindwa kukua na kuongezeka
- uzito kulingana na umri wake
- Kuugua mara kwa mara
- Kupungukiwa damu
- Kupata utapiamlo.

**Ushauri**

Ili kuepukana na matatizo yaliyotajwa hapo juu mtoto hana budi kupata lishe bora tangu anapokuwa tumboni mwa mama yake. Hivyo wazazi wazingatie yafuatayo:-

- Lishe ya Mama Mjamzito

  Mama mjamzito ale chakula bora chenye mchanganyiko wa vyakula vya kujenga mwili, kuupa mwili nguvu na kuulinda mwili. Vyakula hivi viwe vile vinavyopatikana katika eneo anamoishi.





Kielelezo 1.2

- Lishe ya Mtoto

Mtoto anapozaliwa anyonyeshwe maziwa ya mama yake. Maziwa haya humtosheleza mpaka anapofikia umri wa miezi minne. Baada ya umri huo mpe mtoto chakula cha nyongeza na kuendelea kumnyonyesha maziwa ya mama hadi umri wa miaka miwili.



*Kielelezo 1.3*

- Chakula cha nyongeza

Chakula cha nyongeza humfanya mtoto apate shibe ya kutosha. Chakula hiki kitolewe kulingana na umri wa mtoto kama ifuatavyo: –

- Mtoto wa miezi minne hadi sita apewe kidogo kidogo uji laini ulioongezewa mojawapo ya vyakula vifuatavyo: –

Unga wa karanga, unga wa maharage, unga wa soya, unga wa dagaa, maziwa au mayai. Mpe mtoto wako supu ya mboga zinazopikwa nyumbani. Mboga hizo ni kama nyama, maharage, kunde, mbaazi na mboga za majani.

Mpatie mtoto maji ya matunda angalau

mara moja kwa siku. Matunda hayo yanaweza kuwa mapapai, machungwa, mananasi, maembe na mengine yoyote yanayoweza kupatikana. Mlishe mtoto si chini ya mara tano kwa siku.

Mtoto wa miezi sita hadi miaka miwili, alishwe chakula laini cha kawaida na cha kutosha si chini ya mara tano kwa siku. Kumbuka kuwa chakula cha kawaida ni kile kinachotumiwa na familia.

Mtoto wa miaka miwili hadi sita, ale chakula cha kawaida na cha kutosha si chini ya mara tano kwa siku.


## AFYA

Licha ya kumpatia chakula, mtoto ana haki ya kutunzwa kiafya. Afya inahusu kumkinga na maradhi na kumpatia tiba sahihi anapougua

Ili kumkinga mtoto na maradhi, wazazi wanatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo: –

- *Usafi wa Mazingira*

  Daima weka nyumba ya kulala, uwanja unaozunguka nyumba na choo katika hali ya usafi. Mahali anapolala mtoto pawe safi.



*Kielelezo 1.4*

● *Maji ya Kunywa*
Daima hakikisha kuwa maji ya kunywa ya mtoto na familia nzima yanachemshwa.
Mtoto apewe maji ya kunywa kila baada ya kunyonya na kula.
● *Usafi wa Mwili*
Mwogeshe mtoto angalau mara mbili kwa siku. Mvike mtoto mavazi safi yakufaa kulingana na hali ya hewa. Weka nywele za mtoto katika hali ya usafi. Ni vizuri zikiwa fupi ili zitunzwe kwa urahisi. Mkate kucha mtoto kila zinapokuwa ndefu. Anza kumsafisha mtoto meno baada ya kuota. Tumia mswaki laini wa mti.



*Kielelezo 1.5*

**KUMPELEKA KLINIKI**
Mara mtoto anapozaliwa mpeleke kliniki ili akapate huduma zifuatazo: –

Kupimwa uzito ili kuangalia maendeleo ya ukuaji wake na kupata ushauri wa waganga na wakunga.
Kupata chanjo ili kuzuia magonjwa ya kifua kikuu, kupooza, donda koo, kifaduro, pepo punda na surua.

- *Kutumia uzazi wa Mpango (Majira)*

Baba na mama watumie uzazi wa mpango. Kwa kufanya hivyo watakuwa na watoto wachache wa kuwahudumia kikamilifu. Huduma za mpango hupatikana katika kliniki ya mama na watoto iliyoko karibu.

- *Tiba*

Mtoto ana haki kutibiwa vyema kila anapougua. Wazazi wanatakiwa kutekeleza yafuatayo: –

- Mpeleke mtoto zahanati au hospitali mara anapougua.
- Usimcheleweshe mtoto kwa kujaribu kumtibu kienyeji kwani kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha yake.
Epuka kumpeleka mtoto kwa waganga wa kienyeji wasio na vipimo maalum vya tiba.
Epuka sindano na matibabu mengine yanayotolewa majumbani na waganga au watu wasiokuwa na ujuzi.

**Madhara Yatokanayo na Matibabu Yasiyo ya Kitaalamu**

Yafuatayo ni baadhi ya madhara yatokanayo na tiba mbaya: –

- Mtoto kucheleweshwa kupata matibabu sahihi hufanya ugonjwa wake kuzidi au kuwa sugu.
- Matibabu yanayotolewa na watu wasio na utaalam au uangalifu (hasa kuchoma sindano) kunasababisha mtoto kupata majipu, ugonjwa wa manjano na hata UKIMWI.
- Mtoto asipopata matibabu yanayofaa anaweza kufa.

**Umuhimu wa Maji kama Huduma ya Kwanza**

Maji ni muhimu katika kutoa huduma ya kwanza. Kama kila mtu aishie vijijini angelitumia maji vizuri basi magonjwa na vifo vingi hasa kwa watoto wadogo vingalipungua sana.

Hivyo basi wazazi yawapasa kuzingatia utumiaji wa maji kama tiba yao ya kwanza nyumbani kama ifuatavyo: –

- Mnyweshe maji mengi safi na salama mtoto anayeharisha na kutapika, aliye na homa, kuvimbiwa na anayepata choo kigumu.
- Punguza joto la mtoto mwenye homa kali kwa kumpangusa na kitambaa chenye maji.
- Mfukize mvuke wa maji ya moto yenye chumvi mtoto anayekohoa, mwenye pumu, kifaduro, mafua na kichomi (numonia).
- Mkande maji ya uvuguvugu mtoto aliye na maumivu ya misuli na viungo.
- Osha upesi jicho la mtoto lililoingiwa na takataka kwa kutumia maji safi.

## MAHALI PA KUISHI

Mtoto ana haki ya kuishi mahali panapoweza kumkinga na mvua, baridi, jua na upepo. Mahali pa namna hiyo ni nyumba ya kufaa ambayo ina madirisha makubwa yanayoweza kuingiza mwanga na hewa safi.

Malazi ya mtoto yazingatiwe kufuatana na umri wake. Kwa mfano: –

- Mtoto tangu kuzaliwa hadi miaka miwili alale na mama yake hasa anapokuwa mchanga.
- Mtoto afikiapo miaka mitatu anaweza kulala kitanda cha peke yake. Kama haitawezekana, alale na nduguze wakubwa. Lakini hakikisha kwamba nafasi ya kulala ni kubwa ili wasimbane na kumwambukiza magonjwa.
- Wakati wa baridi mtoto apatiwe mavazi na matandiko mazito kumpatia joto.
- Wakati wa joto mtoto apatiwe mavazi na matandiko mepesi.

**Madhara yatokanayo na Kutompatia Mtoto Malazi Bora**

Mtoto anaweza kupata kichomi (numonia), mafua na hata mlipuko wa pumu kama nyumba anamolala itaingiza baridi, unyevunyevu, vumbi, maji na kuvuja kwa nyumba. Watoto wengi wakilala katika chumba kimoja kisichokuwa na madirisha ya kupitisha hewa wanaweza kuambukizana magonjwa, kukosa hewa na kufa.

**Ushauri**

Jenga nyumba kubwa ya kufaa kulingana na mahitaji halisi ya familia. Mpatie mtoto nguo za kuvaa na kujifunika kulingana na hali ya hewa unapoishi.

*Soma vitabu vifuatavyo vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa maelezo zaidi kuhusu malezi ya mtoto.

- Malezi ya Watoto (1987)
- Jiandae Kupata Mtoto (1988)
- Magonjwą ya Hatari kwa Mtoto (1988)

## Sura ya Pili

### HAKI YA KUPENDWA NA KUKUBALIKA

Mtoto anahitaji kupendwa na kukubalika. Wazazi waelewe kwamba kupendwa na kukubalika kwa mtoto huanza tangu mama anapokuwa mjamzito.

### UPENDO

Upendo kwa mtoto ni ile hali ya wazazi kuonyesha furaha mbele ya mtoto. Vile vile wazazi humthamini mtoto kama wanavyojithamini wenyewe.



*Kielelezo 2.1*

**Umuhimu wa Mtoto Kuishi Katika Upendo**

- Ni muhimu wazazi wawe na upendo kwa mtoto wao tangu ujauzito. Hii itawafanya wawe tayari kumpokea anapozaliwa na kumtimizia mahitaji yake.
- Mtoto akiishi katika upendo atapata malezi bora toka kwa wazazi wake. Hii itamwezesha kuwa na afya njema.
- Hujenga tabia ya kupenda wazazi na watu wengine.
- Huwa mwenye furaha.
- Huwa mpole na mtaratibu.

**Sababu za Kukosa Upendo**

Kuna mambo mengi yanayoweza kusababisha mtotc kukosa upendo. Baadhi yake ni:

- Mama akipata mimba wakati usiotegemewa.
- Kuzaliwa kinyume na matarajio ya wazazi kwa mfano, kuzaliwa mtoto wa kiume badala ya wa kike.
- Mtoto kuzaliwa kilema.
- Hali ya kutoelewana kati ya wazazi.
- Wazazi kutomjali mtoto.
- Wazazi kuwa walevi au watovu wa nidhamu.
- Hali ngumu ya uchumi kwa familia.

**Madhara kwa Mtoto Kukosa Upendo**

Mtoto asipopata upendo, anaweza kujenga tabia ya: –

- Kutojiamini,
- Chuki,
- Kukata tamaa,
- Kuwapenda watu wengine wanaoonyesha kumpenda kuliko wazazi wake.
- Kukosa imani kwa wazazi wake.

**Ushauri kwa Wazazi**

Ni muhimu wazazi wamwonyeshe mtoto wao upendo wakati wote. Sio vizuri kwa wazazi kumkaripia mno mtoto akiwa amekosea kwa sababu ataona kuwa wazazi wake

hawampendi. Wazazi waonyeshe upendo kwa mtoto hata kama amekosea.

Ni muhimu pia wazazi kuishi kwa upendo nyumbani. Endapo pana ugomvi kati ya wazazi, chuki isihamishwe kwa mtoto. Vile vile wazazi waepuke kugombana mbele ya mtoto.

**Kukubalika**

Pamoja na kupendwa, mtoto anahitaji kukubalika. Inabidi mzazi amkubali mtoto kama binadamu mwenye haki sawa na binadamu wengine. Mzazi atambue kwamba ana wajibu wa kumkubali mtoto ili aweze kukua katika afya njema na kuwa na maendeleo mazuri.

**Umuhimu wa Mtoto Kukubalika**

Matokeo mazuri ya mtoto kukubalika ni kama yafuatayo: –

- Mtoto atatunzwa vyema kabla ya kuzaliwa
- Baada ya kuzaliwa mtoto atapata malezi bora
- Mtoto atajisikia amelindwa katika familia
- Atakuwa na mwenendo mzuri na upendo kwa wazazi na watu wengine.
- Ataweza kukua na kutumia vizuri vipaji vyake

**Sababu za Mtoto kukosa Kukubalika**

Ipo sababu nyingi zifanuazo mtoto akose kukubalika. Ifuatazo ni baadhi ya sababu hizo: –

- Mama akipata mimba ambayo haikupangwa.
- Kutoelewana au kutengana kwa wazazi wake
- Mtoto kuzaliwa nje ya ndoa.
- Mtoto kuzaliwa na dosari au kilema.

**Madhara kwa Mtoto kukosa Kukubalika**

Mtoto akikosa kukubalika madhara yafuatayo yanaweza kujitokeza: –

- Hakui vizuri na huweza kuonekana mwenye huzuni na wasiwasi.

- Huweza kujenga chuki kwa wazazi wake na watu wengine.
- Hukosa uhuru wa kujifunza na kufanya mambo anayotegemewa katika umri wake.
- Hushindwa kueleza shida zake kwa wazazi.
- Hujiona ametengwa katika familia na hivyo kujenga tabia ya kufanya mambo yake anavyojishauri mwenyewe.
- Huweza kuwa mtovu wa nidhamu.
- Watoto wengine huchukia majina yao na hata wazazi ikiwa majina hayo yana uhusiano na jinsi walivyozaliwa.

**Ushauri kwa Wazazi**

Ili mtoto aweze kukubalika, wazazi wanashauriwa kuzingatia yafuatayo: –

- Wawe na mpango sahihi wa uzazi na hivyo kuepuka kutofautiana katika maamuzi.
- Wajiepushe na tabia ya kuzaa watoto nje ya ndoa.
- Waelewe kwamba mtoto kuzaliwa nje ya ndoa si kosa lake. Hivyo ana haki ya kupata huduma na malezi yanayotakiwa.
- Wajiepushe na tabia ya kuwapa watoto majina yenye uhusiano na jinsi walivyozaliwa.

## Sura ya Tatu

### HAKI YA USALAMA NA KUVUMILIWA

Mtoto ana haki ya kuishi katika hali ya usalama na kuvumiliwa.

### USALAMA

Usalama wa Mtoto ni kuishi katika mazingira ambamo anatunzwa vyema na kuepushwa na vitu vinavyoweza kuhatarisha afya au maisha yake. Ni muhimu mtoto aepushwe na vitu vya hatari. Vitu hivyo ni kama: moto, wanyama, wadudu, madawa, mashimo, madimbwi ya maji, miiba, nyembe, visu na vinginevyo vyenye kuleta madhara akivishika au kuvichezea.

Mtoto h· ɔenda kushika na kula vitu vyote anavyoviona. Ni muhimu wazazi wawe macho sana na nyendo zake. Mtoto aepushwe na bugudha, kelele na vitisho. Vitu hivi vinaweza kuathiri akili, uwezo wa kusikia na ukuaji wake.

**Madhara kwa Mtoto kukosa Usalama**

Mtoto asipolindwa na kuepushwa na vitu vya hatari anaweza kupata madhara ambayo yanaweza kusababisha kifo.



*Kielelezo 3.1*

Mtoto akila vitu kama udongo, nyasi na vinginevyo vichafu, anaweza kupata minyoo, kukwamwa kooni na magonjwa kama kuhara, kutapika na mengineyo.

Mtoto akikuzwa katika mazingira ya kikatili, vitisho, kelele au bugudha, huweza kujenga tabia ya woga na wasiwasi. Vile vile huweza kujenga nidhamu ya woga na kutojiamini katika matendo yake hata anapokuwa mt ·  mzima.

**KUVUMILIWA**

Mtoto anahitaji kuvumiliwa tangu anapozaliwa. Watoto wengine hutokea kuwa na tabia mbalimbali kama utundu, kulialia, kukataa kula, kuuliza maswali mengi na udokozi.

Wakati mwingine mtoto huzaliwa akiwa na dosari au kuugua kwa muda mrefu. Magonjwa mengine hushindikana kupona. Wengine huzaliwa na vilema vya aina mbali mbali. Ulemavu mwingine huwa mkubwa zaidi kiasi cha kutomwezesha mtoto kujimudu hata katika utu uzima.

Kwa hali yoyote ile mtoto ana haki ya kuvumiliwa.

**Sababu zinazofanya Wazazi Wasiwe Wavumilivu**

Kuna sababu nyingi ambazo huwafanya wazazi wasiweze kuwavumilia watoto wao. Sababu hizo ni pamoja na: –

- Kukosa nafasi ya kuwashughulikia watoto kutokana na kazi nyingi.
- Kutokujua madhara yatokanayo na kutowavumilia watoto.
- Kukata tamaa kutokana na matatizo yanayoambatana na ulemavu, ugonjwa wa muda mrefu au usumbufu wa mtoto.
- Kutojali na ulevi.

**Madhara Yatokanayo na Kutovumiliwa**

Mtoto akikosa kuvumiliwa yafuatayo yanaweza kujitokeza: –

- Mtoto hujiona hapendeki wala hajaliwi.
- Mtoto huweza kukosa upendo na nidhamu kwa waza-

zi wake na watu wengine.

- Mtoto huweza kushindwa kujifunza kwa kugundua na kudadisi mambo.
- Mtoto huweza kuwa na tabia ya kiburi na kutoshirikiana na wenzake.

**Ushauri kwa Wazazi**

Wazazi wanashauriwa kuwa wavumilivu kwa watoto wao na kutafuta njia bora za kuwasaidia.

Mtoto atokeapo kuwa na tabia au hali isiyowaridhisha ni vyema wazazi wachunguze chanzo cha hali hiyo. Kwa njia hii wanaweza kumsaidia zaidi mtoto kuliko kuchukua maamuzi ya haraka kama vile kutoa adhabu au kumkemea.

Mzazi kuwa na kazi nyingi isiwe sababu ya kushindwa kumshughulikia mtoto.

Wazazi wanashauriwa kuepukana na tabia ya kutowajali watoto wao. Vile vile wazazi wasiwe walevi ili wasishindwe kujishughulisha na watoto wao.

Ikiwa mtoto ana dosari au kilema au ugonjwa wa muda mrefu ni vema kumwona daktari kwa ushauri.

## Sura ya Nne


### HAKI YA KUJIFUNZA

Mtoto hujifunza tangu anapozaliwa. Hujifunza kwa njia ya vitendo, kuiga na michezo. Hujifunza upesi zaidi anapotumia milango yote mitano ya maarifa ambayo ni kuona, kugusa, kusikia, kuonja na kunusa. Kwa hiyo ni muhimu kwa wazazi kumpatia mtoto haki ya kujifunza. Hatua za kujifunza kwa mtoto zinatofautiana kulingana na umri.

**Umri Tangu Kuzaliwa Hadi Miezi Sita**

Katika umri huu mtoto anajifunza yafuatayo: –

- Kuchezesha viungo vya mwili wake kama vile kutupatupa miguu na mikono.
- Kutabasamu na kucheka
- Kugeuza shingo na kichwa kwa kufuatilia sauti.
- Kufahamu sura ya mama yake na ndugu zake na kutambua sauti zao.
- Kutumia mikono yake kwa kushika vitu vilivyo karibu naye na kuvipeleka mdomoni mwake.
- Kutumia lugha kwa maneno ya kitoto ambayo hayaeleweki.
- Kukaa chini mwenyewe.



*elelezo 4.1*

**Miezi Sita Hadi Mwaka Mmoja**


Wakati huu mtoto anajitunza yafuatayo: –

- Kutambaa na kusimama kwa kushikilia vitu kama vile meza, milango na ukuta.
- Kutumia vitu kama kikombe, kijiko na kata.
- Kudadisi na kuchumguza vitu vinavyomzunguka pale anapoishi.
- Kupenda jamaa zake na wageni.
- Kusema maneno machache.

**Mwaka Mmoja Hadi Miwili**

Mtoto wa umri huu anajifunza: –

- Kutembea na kukimbia
- Lugha
- Kupanda na kushuka kwenye viti na meza bila matatizo
- Kupenda vitu vya rangi
- Kuvutiwa na maongezi ya watu.
- Kuuliza maswali
- Kutambua sauti ya muziki au ngoma.
- Kujua vitu vyake.
- Kujitegemea. Kwa mfano, kula mwenyewe au kuvua viatu vyake.
- Kutengeneza vitu kutokana na udongo, mabua, na nyasi
- Kujivunia vitu vyake.



*Kielelezo 4.2*

**Miaka Miwili hadi Minne**

Katika umri huu mtoto anajifunza yafuatayo: –

- Kuvaa na kuvua nguo
- Maneno mapya na kuongea.
- Kusikiliza hadithi na kuuliza maswali
- Kujionyesha kuwa anajua kila kitu.
- Kuoanisha na kutambua rangi mbalimbali.
- Kucheza na watoto wa rika lake na jinsi yake (kike au kiume) nje ya nyumbani kwao.
- Kutengeneza vitu vyake vya kuchezea na kuvumbua michezo mbali mbali.
- Kutambua mila na desturi,
- Kujenga urafiki na wenzake
- Kwenda chooni kujisaidia mwenyewe.



*Kielelezo 4.3*

**Miaka Minne Hadi Sita:**

Mtoto katika umri huu anajifunza: –

- Kusaidia shughuli ndogo ndogo za nyumbani hasa za jikoni..
- Kutofautisha neno/jambo la kweli au la uongo
- Kutambulika anapofanya vitu kama vile kusifiwa, kupongezwa na kupewa pole anapostahili.
- Kucheza zaidi nje ya nyumbani kwao na mzazi akiondoka au kumuacha hamlilii.
- Kushirikiana vitu vyake na marafiki zake.

**Miaka Saba na Kuendelea**

Kuanzia umri wa miaka saba na kuendelea mtoto anapaswa kuanza masomo katika shule ya Msingi. Huko atajifunza kusoma, kuandika, kuhesabu na masomo mengine. Masomo hayo yatasaidia katika kumuandaa mtoto kwa maisha ya kujitegemea hapo baadaye. Pia ataendelea kujifunza utu unaohusu tabia nzuri kama ushirikiano, upendo, na jinsi ya kuishi pamoja kijamaa.

**Umuhimu wa Mtoto Kujifunza**

Mtoto akipatiwa nafasi ya kujifunza anaweza: –

- Kutumia akili yake vizuri.
- Kushirikiana na wenzake vizuri
- Kukuza na kutumia vipaji vyake mbalimbali.
- Kutatua matatizo yatokanayo na mazingira yake
- Kujitegemea
- Kujiendeleza yeye mwenyewe pamoja na jamii yake.

**Madhara Yatokanayo na Kutopewa Nafasi ya Kujifunza**

Iwapo mtoto hatapata nafasi ya kujifunza anaweza kuchelewa;

- Kutembea,
- Kuzungumza,
- Kuimarisha viungo vyake,
- Kujitegemea,

- Uwezo wa kufikiri,
- Uwezo wa kuvumbua vitu,
- Kuwa na ushirikiano na wenzake.

**Ushauri kwa Wazazi**

Mtoto anajifunza zaidi anapotumia milango yote mitano ya maarifa ambayo ni kuona, kugusa, kusikia kuonja na kunusa. Mtoto hujifunza kwa njia ya kuiga na michezo, kwa hiyo wazazi wanashauriwa: –

- Kuhakikisha kuwa mahali anapochezea mtoto ni salama.
- Mtoto apatiwe vifaa mbali mbali vya kuchezea kulingana na umri wake. Vifaa hivyo viwe vile vinavyopatikana katika mazingira yake.
- Wazazi na watu wengine wazungumze na mtoto uso kwa uso na watamke maneno vizuri ili kumwezesha mtoto kujifunza lugha.
- Wazazi wamfundishe mtoto tabia nzuri na wawe mfano kwake.
- Kumsikiliza mtoto ili wajue mahitaji yake na kumtimizia. Wajibu maswali yake kwa lugha rahisi inayoeleweka.
- Kumpeleka mtoto katika vituo vya kulelea watoto ili ajumuike na wenzake.
- Kushirikiana na mwalimu kumuendeleza mtoto.
- Kumsimulia mtoto hadithi na nyimbo ambazo zitamfundisha lugha, mila na desturi za jamii.
- Wazazi wafuatilie maendeleo ya kukua kwa mtoto. Wampe sifa na kumrudi inavyostahili.
- Kumpeleka mtoto wao shule ya msingi afikapo umri wa miaka saba.
- Kujihusisha na maendeleo ya mtoto wao shuleni kwa kufuatilia na kuchunguza daftari zake za shule na mwenendo wake.
- Kumpatia mahitaji mbali mbali ya shule kama: –
  Sare ya shule

Vitabu na kalamu
Madaftari
Mfuko wa kuchukulia daftari
Kumpatia chakula cha kutosha kabla ya kwenda shule na baada ya kurudi kutoka shuleni.

## Sura ya Tano

## HAKI YA UHURU WA KUTENDA NA KUJIELEZA

Wazazi wengi wanaamini kuwa mtoto mdogo anapaswa kulindwa kila wakati. Wanaamini kuwa mtoto akipewa uhuru wa kutenda, usalama wake utakuwa hatarini. Pia atakuwa mharibifu. Aidha akipewa uhuru wa kujieleza atakuwa msumbufu na atakosa adabu njema. Huamini kuwa mtoto mwenye adabu njema ni mtulivu, hauliziulizi maswali na hazungumzi hovyo mbele ya wakubwa. Vile vile husema kuwa mtoto mdogo hana ujuzi wa mambo mengi.

Imani hiyo hufanya wazazi wengi wamchunge mtoto wao kupita kiasi. Kwa hiyo humnyima nafasi ya kudadisi mazingira yake. Wengine huamua kumfungia mtoto nyumbani na kumpimia eneo la kucheza.


Imani hiyo siyo nzuri. Mtoto ana haki ya kupewa uhuru wa kutenda na kujieleza.

**Uhuru wa Kutenda**

Kwa kawaida mtoto anapenda kurusharusha miguu na mikono yake, kushika hiki na kile, kukimbia na kurukaruka. Anapenda kuzunguka zunguka sehemu zote ndani na nje ya nyumba. Hufanya vitendo mbalimbali vinavyomfurahisha. Vitendo hivyo hutofautiana kulingana na umri.

Umuhimu wa Mtoto Kupewa Uhuru wa Kutenda ni muhimu Inabidi: -

- Kujifunza na kugundua mambo ambayo hakuyafahamu kabla
- Kupata nafasi nzuri ya kuyafahamu mazingira yake.
- Kutumia akili yake kufikiri
- Kuamsha hamu ya kuweza kuona, kutenda na kufahamu mambo mengi.



*Kielelezo 5.1*

Uhuru wa kutenda pia humsaidia mtoto kujenga tabia ya udadisi. Tabia hii humfanya ajifunze haraka. Huwa mwepesi kuyaelewa mambo. Hujenga hali ya kujiamini na ujasiri.

**Madhara Yatokanayo na Kutopewa Uhuru wa Kutenda**

Iwapo mtoto hatapewa uhuru wa kutenda tangu udogo wake anaweza: –

- Kutokua haraka
- Kutojenga tabia ya udadisi na uvumbuzi
- Kuwa mnyonge na kujenga tabia ya woga.
- Kujenga tabia ya kutojiamini.

Hali hii inaweza kuendelea hadi ukubwani na kumfanya ashindwe kushirikiana na watu wengine.

**Ushauri kwa Wazazi**

Ili kuhakikisha kuwa mtoto anajijengea misingi ya udadisi na kupenda kujifunza, wazazi wanashauriwa—

- kumpatia mtoto uhuru wa kutenda na kufanya yale yatakayomsaidia kukuza akili na mwili wake kulingana na umri wake.
- Kuwapa watoto moyo wanapotenda kitu kipya.
- Kutomchunga mtoto kupita kiasi.
- Kujenga urafiki na mtoto wao.
- Kukubaliana na vitendo vya mtoto wao kulingana na maisha ya sasa.

## UHURU WA KUJIELEZA

Kwa kawaida mtoto anapenda kupata maelezo kwa kila jambo analoliona. Vile vile kujieleza na kutaka kueleweka kwa kila jambo linalotokea.

Mtoto mchanga hujieleza kwa vitendo. Kwa mfano, mtoto akiwa na njaa, akijikojolea au anapotaka kusinzia analia ili kueleza shida yake.

Mtoto akishaanza kuzungumza hupenda kufafanuliwa kila analoliona na kuuliza maswali mengi. Huwa na hamu ya kujifunza mambo mapya.

Wazazi wengine huchukulia kitendo hiki kuwa ni usumbufu na ukosefu wa adabu. Hivyo humwacha mtoto wao na hamu ya kutaka kufahamu mambo.

**Umuhimu wa Kupewa Uhuru wa Kujieleza**

Wazazi hawana budi kufahamu kuwa mtoto ana mambo anayyaona ambayo anapenda apate maelezo na ufafanuzi wake. Mtoto akipewa uhuru wa kujieleza inakuwa rahisi kwake kujenga hali ya:-

- Urafiki,
- Uhuru wa kutoa mawazo,
- Kujiamini,
- Ujasiri,
- Upendo na ushirikiano.

Vile vile ni nafasi nzuri kwa wazazi kuweza kumwelewa mtoto wao. Kadhalika wazazi wanaweza kugundua kama mtoto wao anaendelea vizuri au ana matatizo na dosari katika makuzi yake.

**Madhara Yatokanayo na Kutopewa Uhuru wa Kujieleza**

Iwapo mtoto hatapewa uhuru wa kujieleza tangu udogo wake, tabia na mwenendo wake vinaweza kuwa na dosari. Dosari hizo zinaweza kuendelea hata utakapokuwa mkubwa. Mtoto anaweza kujenga:-

- Tabia ya woga
- Hali ya kutojiamini
- Hali ya wasiwasi hasa anapozungumza na watu wakubwa
- Tabia ya kutokuwa mkweli
- Hali ya upweke na kuona kuwa anakataliwa.
- Kutoweza kujieleza.

**Ushauri kwa Wazazi**

Ili kuhakikisha kuwa mtoto anajijenea tabia ya udadisi, uhuru wa kujieleza na kuuliza maswali, wazazi wanashauriwa:-


- Kuhakikisha kuwa wanapata muda wa kuongea na kujadiliana na mtoto wao.
- Kumjibu mtoto maswali anayouliza na kumsikiliza anapojieleza.
- Kuwa rafiki wa mtoto wao ili asiwaogope.
- Kujua kuwa mtoto anapokaa kimya si dalili ya utulivu au tabia njema. Huenda mtoto ana matatizo au dosari katika makuzi yake. Pengine amefadhaika kwa sababu wazazi wameshindwa kumpa nafasi ya kujieleza.
- Kuzingatia kuwa mazingira waliyokulia wao ni tofauti na maisha ya sasa.

Pamoja na hayo haina maana kuwa mtoto ana haki ya kufanya hata yale yasiyokubalika. Mtoto ana haki ya kuwa huru kujieleza chini ya uongozi na ushauri wa wazazi kwa kuzingatia misingi inayokubalika na jamii.

## Sura ya Sita

### HAKI YA KUONGOZWA NA KUSHAURIWA

Ili kujenga tabia na mwenendo unaokubaliwa katika jamii, ni wajibu wa wazazi kumuongoza na kumshauri mtoto wao.



*Kielelezo 6.1*

Baadhi ya wazazi hawajali mwenendo wa mtoto wao tangu anapokuwa mdogo. Humwacha afanye kila kitu bila uongozi wowote.

Humtegemea mtoto huyo kuwa na mwenendo wanaoutaka wao bila kumwongoza, kumwelekeza na kumshauri.

Mtoto anapokwenda kinyume cha matarajio ya wazazi, hupigwa au hupewa adhabu kali bila maelezo.

Mtoto hazaliwi akiwa anajua kila kitu. Hajui mila wala desturi.

Kwa sababu hiyo, mtoto ana haki ya kuongozwa na kushauriwa.

**Umuhimu wa Kuongozwa na Kushauriwa**

Kila mtoto ana utu wake wa kipekee. Utu huo hutegemea mazingira anamokulia. Vitendo afanyavyo, yale anayoyaona, kuyasikia, kuyapitia na watu wote anaowafahamu husaidia kujenga utu wake.

Mtoto hazaliwi na tabia njema au mbaya. Tabia hujengwa katika maisha yake na wazazi, ndugu na jamii kwa ujumla.

Wazazi wanalo jukumu kubwa la kumwongoza, kumwelekeza na kumshauri mtoto.

Hii itamwezesha kutambua jema na baya na kuzifahamu mila na desturi zinazokubalika kijamii.

Wazazi wanao wajibu wa kumwelewesha mtoto umuhimu wa kutunza na kuthamini vitu vyake vyote anavyotumia.

Kwa mfano, vifaa vya kuchezea, vifaa vya nyumbani na vifaa vya shuleni. Hii itamjengea tabia na mwenendo mzuri wa kuheshimu vitu na watu.

**Madhara Yatokanayo na Kukosa Uongozi na Ushauri**

Madhara mbali mbali yanaweza kutokea kwa mtoto iwapo atakosa maelekezo na ushauri. Madhara hayo yanaweza kuwa:-

- Mtoto kufanya mambo yake kwa kubuni na kujaribu jaribu tu.
- Kuiga tabia mbaya.
- Kutoweza kujiamini
- Mwenendo mbaya na uwezo mdogo wa kufikiri
- Kuwa mtukutu
- Kutojali na kutowajibika
- Kutoelewana na wenzake
- Kukosa ushirikiano
- Tabia ya udanganyifu, ukaidi na wizi.

**Ushauri kwa Wazazi**

Mtoto anapokosea au kuonyesha tabia ya utukutu wazazi wanapaswa kutafuta sababu za mtoto kutenda kosa hilo.

Baada ya hapo wamshauri na kumweleza ubaya wa kosa hilo. Pia wamweleze madhara yanayoweza kutokea kufuatana na kosa hilo. Kumkanya kwa kumweleza na kumwelewesha kutamwezesha kutambua zuri na baya.

Wazazi wengine hupendelea kumpiga mtoto badala ya kumwelewesha anapofanya kosa. Kumpiga mtoto siyo njia pekee ya kumrudi. Inaweza kumuumiza na pengine kusababisha kilema cha maisha.

Vile vile kupiga kunaweza kusababisha mtoto kuwa sugu. Wakati mwingine kunaweza kusababisha mtoto kuwa na nidhamu ya woga.

Inapobidi kutoa adhabu kwa mtoto wazazi wanatakiwa wazingatie yafuatayo:-

- Adhabu itolewe mara tu baada ya kosa ili mtoto aweze kuhusisha kosa na adhabu.
- Adhabu isitolewe kwa ukali au ukatili.
- Adhabu iwe ya kujenga na kuhimiza tabia njema.
- Mtoto aelezwe sababu ya kuadhibiwa ili aone au aelewe kwamba adhabu hiyo ni sawa na ya haki.
- Adhabu isiwe ya kumuaibisha mtoto na kusababisha chuki.
- Kama mtoto ataendelea kuonyesha tabia mbaya licha ya ushauri wa wazazi, basi wazazi wasikate tamaa.
- Watafute msaada na ushauri wa wataalamu wa malezi ya watoto, na wengine wanaoweza kusaidia.

Ikumbukwe kwamba, matatizo ya namna hiyo pengine yasingetokea iwapo kama mtoto angepewa maelekezo na ushauri unaositahili kwa wakati unaositahili. Kwani wahenga walisema ''Samaki mkunje angali mbichi''.

## Sura ya Saba

### HAKI ZA MTOTO KIKATIBA NA KISHERIA

Haki za watoto zinalindwa kisheria ulimwenguni kote. Kila nchi duniani imeweka sheria maalum kulinda haki za watoto. Katika Tanzania, haki za watoto zinalindwa kikatiba na kisheria.

**Haki za mtoto kikatiba**

Katiba ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inaeleza kwamba binadamu wote ni sawa. Mtoto ni mwanadamu sawa na wanadamu wengine. Hivyo ana haki ya kupata mahitaji yote sawa na binadamu wengine.

Chini ya Katiba hiyo, vijana wamepewa nafasi ya kushiriki katika maamuzi na shughuli mbalimbali za kitaifa chini ya Jumuiya ya Vijana na Chipukizi.

**Haki za mtoto kisheria**

Katika sheria za Tanzania, vipo vifungu maalum kuhusu haki za watoto. Hivyo mambo ambayo mtoto hufanyiwa kinyume na sheria hizo hatua za kisheria huweza kuchukuliwa. Wazazi wanao wajibu wa kuzingatia na kufuata maagizo ya sheria zifuatazo

Haki ya Kutunzwa na Wazazi Wake. Katika Tanzania, sheria inamlinda mtoto kutunzwa na wazazi wake tangu akiwa tumboni mwa mama. Kifungu cha 150 – 152 cha kanuni ya adhabu kinazuia utoaji wa mimba.

Kitendo chochote cha makusudi kinachoweza kusababisha mimba kutoka ni kosa la jinai kwa mtu anayetoa mimba au kusaidia mimba itoke. Mume au mke akipatikana na kosa la kusababisha mimba itoke au kutoa mimba anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria. Adhabu ya kifungo huweza kutolewa.

Vile vile ikibainika kwamba mtoto angezaliwa hai lakini ikashindikana kutokana na uzembe, hatua za kisheria

huweza kuchukuliwa kwa mwenye kufanya uzembe huo.

Mtoto akishazaliwa hai, sheria inamlinda maisha yake yote. Kudhuru maisha ya mtoto aliyezaliwa hai ni kosa la jinai na adhabu yake ni kifungo au kunyongwa.

Mtoto akishazaliwa ana haki ya kutunzwa na wazazi wake hadi kufikia umri wa kujitegemea. Sheria ya ndoa ya mwaka 1975 inampa mtoto haki ya kupatiwa mahitaji yake yote muhimu kwa maisha yake.

Katika sheria hii mama anayelea watoto anayo haki ya kisheria ya kupata mahitaji yote muhimu toka kwa mume wake. Mume akikosa kufanya hivyo makusudi huweza kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kifungu cha 207 cha kanuni ya adhabu kinazuia vitendo vya kumnyima mtoto mahitaji muhimu. Vitendo vinavyozuiwa ni pamoja na kumnyima mtoto chakula, kukosa kumpatia matibabu anapougua, kukosa kumpatia mavazi na malazi. Adhabu ambayo huweza kutolewa kwa kosa hilo ni kifungo au faini.

Ni kosa vile vile kukosa kutoa huduma muhimu kwa mtoto baada ya kuvunjika kwa ndoa. Mzazi anayekosa kufanya hivyo huweza kupoteza haki ya kummiliki mtoto huyo.

**Haki ya Kupatiwa Elimu**

Mtoto anayo haki ya kisheria kupatiwa elimu ya msingi. Haki hii imeelezwa katika sheria ya Elimu ya Taifa ya mwaka 1976.

Sheria hii inaagiza kwamba mtoto akishafikia umri wa kwenda shule wazazi wake lazima wampeleke shule. Mzazi akikosa kufanya hivyo huweza kuchukuliwa hatua za kisheria. Adhabu ya faini au kifungo huweza kutolewa.

Wakati mwingine faini na kifungo huenda pamoja. Kosa kama hilo likifanyika mara ya pili adhabu huongezeka mara mbili vile vile.

Ni kosa vile vile kwa mtu yeyote mbali ya mzazi kusababisha mtoto aliye chini ya malezi yake asiende shule.

Adhabu ya faini au kifungo huweza kutolewa kwa kosa hilo.

Wazazi wengine hukatisha masomo ya watoto. Hii hufanyika kwa kumpa mtoto kazi nyingine kama kufanya biashara, kuchunga mifugo, kumwoza na nyinginezo. Sheria inazuia kitendo chochote kwa mzazi au mtu mwingine kukatisha masomo ya mtoto.

Watoto wengine hushindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya kukosa mahitaji muhimu kama sare ya shule, vitabu, kalamu na madaftari. Mzazi anayepuuzia kutoa huduma hizo kwa makusudi huweza kuchukuliwa hatua za kisheria.

Sheria vile vile imeweka utaratibu wa kumwachisha mtoto masomo iwapo tabia yake imeshindikana kuvumiliwa. Kwa utaratibu huu, uamuzi wa kumwachisha mtoto masomo huchukuliwa na kamati au bodi ya shule na siyo mwalimu peke yake.

Chini ya kifungu cha uachishaji na ufukuzaji wa watoto shuleni, watoto watukutu walioshindikana shuleni hupelekwa kwenye shule ya maadilisho iliyoko Irambo, Mkoa wa Mbeya.

**Haki ya Kutonyanyaswa**

Ni kosa la jinai kumnyanyasa mtoto. Vitendo vya kikatili au kumdhalilisha utu wake vimezuiliwa. Baadhi ya vitendo ambavyo vimezuiliwa kisheria ni kama: –

- Kumpiga kwa kumwonea mtoto
- Kumpiga na kumuumiza mtoto.
- Kumzini mtoto mwenye umri chini ya miaka 14..
- Kumbaka mtoto (kumzini kwa nguvu)
- Kumpa mimba mtoto wa shule
- Kumshirikisha mtoto katika vitendo vya umalaya
- Kumtorosha mtoto toka kwa wazazi wake.
- Kumuuza au kumnunua mtoto.
- Kumdanganya au kumshawishi mtoto kufanya makosa.

Haki nyingine za watoto zinalindwa na sheria za kazi. Kwa mfano, sheria ya uajiri inakataza kuwaajiri watoto wadogo chini ya umri wa miaka 14.

Vile vile sheria inazuia kumwajiri mtoto katika kazi ambayo inaweza kuhatarisha afya au maendeleo yake.

Kuna mambo ambayo hayajatungiwa sheria lakini yakifanyika hudhalilisha utu wa mtoto. Baadhi ya mambo hayo ni: –

- Kukata kimeo
- Kutoa meno
- Kukata masikio
- Kutahiri watoto wa kike na mengineyo.

**Ni muhimu wazazi wazielewe sheria hizo na kuzifuata.**

Kimepigwa Chapa na Printfast (T) Ltd. Dar es Salaam